Daudi Alijipatia Nguvu katika Bwana Mungu Wake

(David Strengthened Himself in the Lord His God)

na

Ellis P. Forsman

Daudi Alijipatia Nguvu katika Bwana Mungu Wake

na

Ellis P. Forsman

Octoba 11, 2011

Daudi Alijipatia Nguvu katika Bwana Mungu Wake

1 Samweli 30:6

Unafanya nini cha kwanza wakati huu wa shida?

Kila mmoja ana matatizo wakati hadi wakati, lakini siyo kila mtu anajaribu kusuluhisha matatizoa yake kwa wakati uo huo.

Ni njia IPI nzuri?

Mtu mmoja katika Biblia aliyekuwa na matatizo zaidi alikuwa ni Daudi.

Kwa mfano:

- Alifuatwa na mfalme Sauli.
- Alikimbia majaribio maengi ya kuuawa.
- Alichukua muda mwingi kujificha jangwani.
- Katika tukio moja familia yake yote ilitekwa.
- Marafiki zake walimgeuka na kutaka kumwua.
- Alikumbwa na aibu na kuzini na kuuwa.
- Kijana wake Amnoni alimbaka mbinti yake Tamari.
- Kijana wake mwingie Absalomu alimuua Amnoni.
- Absalomu aliongoza mapinduzi dhidi ya baba yake.
- Absalomu mwenyewe aliuawa, ikawa maumivu zaidi kwa Daudi. Unahitaji niendelee? Hakika Daudi alikuwa binadamu mwenye matatizo mengi!

Alafu kidogo, aliyashinda yote na amekuwa akikumbukwa kama "*mtu mwenye moyo wa Mungu.*" Aliwezaje kufanya hili?

Tutapata jibu tunapoendelea kuangalia alichokifanya Daudi alipokabiliwa na moja ya matatizo makubwa, kama ilivyoandikwa katika…

1 Sam. 3:1-6, "*Ikawa Daudi na watu wake walipokuwa wamefika Siklagi siku ya tatu, hao Waamaleki walikuwa wameshambulia Negebu, na Siklagi, nao wameupiga Siklagi na kuuchoma moto; nao wamewachukua mateka wanawake walio kuwamo wakubwa kwa wadogo; hawakuua wo wotw ila wakawachukua wakaenda zao. Basi Daudi na watu wake walipoufikilia mji, tazama ulikuwa umechomwa moto; na wake zao, na watoto wao, waume kwa wake wamechukuliwa mateka. Ndipo Daudi na watu waliokuwa pamoja naye wakainua sauti zao na kulia, hata walipokuwa hawana nguvu za kulia tena. Na hao wake wawili wa Daudi walikuwa wamechukuliwa mateka, Ahinoamu wa Yezreeli, na Abigaili, aliyekuwa mkewe Nabali wa Karmeli. Naye Daudi akafadhaika sana kwa sababu watu walikuwa wakisema kwamba apigwe kwa mawe, kwa maana nafsi zao hao watu walisononeka, kila mtu kwa ajili ya wanawe na binti zake; lakini Daudi alijitia nguvu katika BWANA, Mungu wake.*"

Alichokifanya Daudi wakati wa shida

Mazingira ya 1 Sam. 30:1-6. Kwa wakati huu katika maisha yake, Daudi alikuwa aanaishi Siklagi kusini mashariki mwa ukanda wa Gaza.

Baada ya kukimbia kutoka kwa Mfalme Sauli; na sasa alikuwa amekabiliwa na Wafilist (Goliathi alikuwa Mfilisti).

Wafilisti walikuwa wanajianda kupigana na Mfalme Sauli, na Daudi na watu wake walikwenda kuungana na Wafilisti (kusini mashariki mwa pwani ya bahari ya Mederenia, pamoja na ukanda wa Gaza).

Lakini Wafilisti hawakumwamini Daudi kikamilifu, hivyo wakamrudishaa yeye na watu wake huko Siklagi.

Tukisoma 1 Sam. 301-6, tunapata kwamba:

- Kwamba mji wa Siklagi umevamiwa na kuchomwa na Waamaleki (Wa-ama-leki) (kusini mwa Siklagi) (ms.1).
- Wanawake na watoto walitekwa nyara, pamoja na wale wa familia yake (mis. 2-5).

Kiuhalisia Daudi amechanganyikiwa; lakini pamoja na hili, watu wako tayari kumuua kwa kutokuwepo pale walipomhitaji. (ms. 6)

Lakini angalia kwa makini sehemu ya mwisho ya msitari wa sita. Daudi anafanya nini baada ya kuipoteza familia yake, na maisha yake mwenyewe yanatishiwa?

Maandiko katika msitari wa 6 inasema:

- 1 Sam. 30:6, "*…Daudi alijitia nguvu katika BWANA Mungu wake.*"
- 1 Sam. 30:6 (NKJV), "*Lakini Daudi alijitia nguvu katika BWANA Mungu wake.*"

Hiki ndicho Daudi alifanya kwanza wakati wa shida… Alijitia nguvu katika Bwana Mungu wake! Kwa nguvu aliyopokea, alikuwa tayari kukabiliana na matatizo yoyote ambayo yalikuwa mbele yake.

Lakini inamanisha nini "*fariji* (tia nguvu) *katika Bwana Mungu*"? katika jitihada za kujibu swali hili, tunaipata kwamba inamsaada kuzingatia kwamba baadhi ya Zaburi iliandikwa na Daudi wakati wa matatizo.

Daudi alijitia vipi nguvu katika Bwana Mungu wake

Wakati huu wa shida, mara zote Daudi alitunga zaburi.

Akifuatiwa na Saulo, aliandikaa Zaburi 59, Zaburi 59:1-4, "*Ee Mungu uniponye na adui zangu, uniinue juu yao wanaoshindana nami. Uniponye nao wafanyao maovu, uniokoe na watu wa damu. Kwa maana wanaiotea nafsi yangu; wenye nguvu wamenikusanyikia; Ee BWANA, si kwa kosa langu, wala si kwa hatia yangu. Bila kosa langu huenda mbio, hujiweka tayari; uamke uonane nami nakutazama.*"

Alipofungwa katika Gathi ya wafilisti, aliandika Zaburi 56. Zaburi 56:1-2, "*Mungu unirehemu, maana yuko atakaye kunimeza, mchana kutwa ananionea akileta vita. Adui zangu wanataka kunimeza mchana kutwa, maana waletao vita juu yangu kwa kiburi ni wengi.*"

Akitoroka kutoka kwa Abisalomu, kijana wake, aliandika Zaburi 3. Zaburi 3:1-2, "BWANA watesi wangu wamezidi kuwa wengi, ni wengi wanaonishambulia, ni wengi wanaoiambia nafsi yangu, hana wokovu huyu kwa Mungu."

Akijificha katika jangwa la Yudea, aliandika Zaburi 63. Zaburi 63:1-11, "*Ee MUNGU Mungu wangu nitakutafta mapema, nafsi yangu inakuonea kiu, mwili wangu wakuonea shauku, katika nchi kame na uchovu, isiyo na maji. Ndivyo nilivyokutazama katika patakatifu, nizione nguvu zako na utukufu wako. Maana fadhili zako ni njema kuliko uhai; midomo yangu itakusifu. Ndivyo nitakavyokubariki maadamu ni hai; kwa jina lako nitainua mikono yangu. Nafsi yangu itakinai kama kushiba mafuta na vinono; kinywa change kitakusifu kwa midomo ya furaha. Ninapokukumbuka kitandani mwangu nakutafakari wewe makesha yote ya usiku. Maana wewe umekuwa msaada wangu na uvulini mwa mbaya zako nitashangilia. Nafsi yangu inakuandama sana; mkono wako wa kuume unanitegemeza. Bali waitafutao nafsi yangu ili kuiharibu, wataingia pande za nchi zilizo chini. Watatolewa wafe kwa nguzu za upanga, watakuwa riziki za mbwa-mwitu. Bali mfaalme atamfurahia Mungu, kila aapaye kwa yeye atashangilia, kwa maana vinywa vya waongo vitafumbuliwa.*"

Kutoka ktika zaburi hizi, tunaweza kujifinza jinsi Daudi alivyojitia nguvu katika Bwana Mungu wake.

Kutoka katika Zaburi 56, tunajifunza kwamba Daudi aliweka tumaini lake kwa Mungu ili amsaidie.

- Zaburi 56:3-4, "*Siku ya hofu yangu nitakutumaini wewe; kwa msaada wa MUNGU nitalisifu neno lake. Nimemtumaini Mungu sitaogopa; mwenye mwili atanitenda nini.*"
- Zaburi 56:9-11, "*Ndipo adui zangu watarudi nyuma siku ile niitapo. Neno hili najua kuwa MUNGU yu upande wangu; kwa msaada wa MUNGU nitalisifu neno lake. Kwa msaada wa BWANA nitalisifu neno lake.*"

Kutoka katika Zaburi 59, tunajifunza kwamba Daudi alikusudia kuendelea kumsifu Mungu kwa msaada wake. Zaburi 59:16-17, "*Nami nitaziimba nguvu zako asubuhi, nitaziimba fadhili zako kwa furaha. Kwa kuwa ndiwe uliyekuwa ngome yangu, na makimbilio siku ya shida yangu. Ee nguvu zangu, nitakuimbia kwa furaha, maana Mungu ndiye aliye ngome yangu, Mungu wa fadhili zangu.*"

Kutoka Zaburi 63, tunaona kwamba Daudi kwamba Daudi *nitakutafuta mapema* alishinda tatizo lake la upweke kwa:

Akimtafta Bwana. zaburi 63:1-2, "*Ee MUNGU, Mungu wangu, nafsi yangu inakuonea kiu, mwili wangu wakuonea shauku, katika nchi kame na uchovu, isiyo na maji. Ndivyo nilivyokutazama katika patakatifu, nizione nguvu zako na utukufu wako.*"

Akisifu na kuomba. Zaburi 63:3-5, "*Maana fadhili zako ni njema kuliko uhai; midomo yangu itakusifu. Ndivyo nitaakavyokubariki*

madamu ni hai; kwa jina lako nitainua mikono yangu. Nafsi yangu itakinai kama kushiba mafuta na vinono; kinywa changu kitakusifu kwa midomo ya furaha."

Akimtafakari Bwana. Zaburi 63:6-7, "*Ninapokukumbuka kitandani mwangu, nakutafakari wewe makesha yote ya usiku. Maana wewe umekuwa msaada wangu, na uvulini mwa mbawa zako nitashangilia.*"

Katika kila moja ya zaburi hizi, Daudi kimsingi anazungumzia jambo linalofanana…

- Wakati wa shida, weka tumaini lako kwa Bwana.
- Kaa karibu naye, katika kumsifu na kumuomba.
- Fanya hili, nawe utafanywa imara Bwana anapokuegemeza.

Zaburi 63:8, "*Nafsi yangu inakuandama sana; mkono wako wa kuume unanitegemeza.*"

Hivi ndivyo ambavyo "*Daudi alivyojitia nguvu kwa Bwana Mungu wake*" na alikuwa tayari kukabiliana na matatizo yake na aliyashinda kwa msaada ambao Bwana alimpa.

Vipi kuhusu sisi leo? Nyakati za shida, je tunafuata mfano wa Daudi? Zingatia mawazo haya…

Kuhusiana na matatizo yetu leo

Tunakumbana na shida nyingi, hata kama Wakristo. Mengine yanahusiana na familia, au matatizo mengine binafsi; mengine yanahusiana na kazi, na matatizo ya kifedha; na mengine yanahusiana yanayotokea kanisani.

Katika shauri lolote, watu hujaribu kuyasshughulikia wenyewe au wanakimbia chanzo cha matatizo. Wanamwacha Mungu kabisa kutoka kwenye maandiko. Wakati mwingine wanamwacha kabisa; hawamsifu na kumwomba kila siku; wakiacha makusanyiko tunayokutana ili kuhimizana kila mmoja kwa mwenzake na kumwabudu Mungu.

Sababu mara nyingi hutolewa hivi:

Kama tatizo ni la binafsi, "Ngoja nitengeze maisha yangu, alafu nitaweza kumtumikia Mungu na kumwishia."

Kama tatizo limesababishwa na mtu mwingine, "Siwezi kuwa pamoja na fulani, hivyo nitaondoka tu."

Lakini unajua, Mungu anachukia tunapotatua matatizo yetu bila kumhusisha! Mungu anamchukulia mtu kama huyo kama amelaniwa!

Yer. 17:5-8, "*BWANA asema hivi amelaaniwa mtu yule amtegemeaye mwanadamu, amfanyaye mwanadamu kuwa kinga yake na moyoni mwake amemwacha BWANA. Maana atakuwa kama fukara nyikani, hataona yatakapotokea mema; bali atakaa jangwani palipo ukame, katika nchi ya chumvi isiyokaliwa na watu. Amebarikiwa mtu yule anayemtegemea BWANA, ambaye BWANA ni tumaini lake. Maana atakuwa kama mti uliopandwa kando ya maji, uenezao mizizi yake karibu na mto; hautaona hofu wakati wa hari ujapo, bali jani lake litakuwa bichi; wala hautahangaika mwaka wa uchache wa mvua, wala hautaacha kuzaa matunda.*"

Mfano mzuri wa Mungu kutopendezwa wakati watu wake wanaposhindwa kumtafuta kwa ajili ya nguvu inayopatikana katika Isaya.

Aliposhambuliwa na Waashuru (Iraq leo), Israeli iliweka tumaini lake kwa Misri. Isa. 30:1-2, "*Ole wao watoto waasi; asema BWANA; watakao mashauri lakini hawayataki kwangu mimi; wajifunikao kifuniko lakini si cha roho yangu; wapate kuongeza dhambi juu ya dhambi; waendao kutelemkia Misri wala hawakuuliza kinywani mwangu; ili wajitie nguvu kwa nguvu za Farao, na kutumainia kivuli cha Misri.*"

Kwa sababu hii, Mungu alihaidi kushangaza juhudi za Israeli ili kusuluhisha matatizo yao wenyewe, au wamtafute jirani yao mmoja, hasa yule ambaye wakati fulani alikuwa adui yake!

- Isa. 30:3, "*Basi nguvu za Farao zitakuwa aibu yenu, na kutumainia kivuli cha Misri kutakuwa kufadhaika kwenu.*"
- Isa. 31:1-3, "*Ole wao watelemkao kwenda Misri wapate msaada, na kutegemea farasi; watumainio magari kwa kuwa ni mengi, na wapanda farasi kwa kuwa ni hodari sana; lakini hawamwangalii Mtakatifu wa Israeli, wala hawamtafuti BWANA! lakini yeye naye ana akili, naye ataleta uovu wala hatayatangua maneno yake; bali ataondoka juu ya nyumba yao watendao mabaya, na juu ya msaada wa hao watendao maovu. Basi Wamisri ni wanadamu wala si Mungu, na farasi zao ni nyama wala sir oho; na BWANA atakaponyosha mkono wake, yeye asaidiaye atajikwaa, nay eye asaidiwaye ataanguka, nao wote pamoja watakoma.*"

Ndiyo, Mungu alitaka Israeli imtumainie, na siyo katika wao wenyewe.

Isa. 30:15-16, "*Kwa maana Bwana MUNGU, Mtakatifu wa Israeli, asema hivi, kwa kurudi na kustarehe mtaokolewa; nguvu zenu zitakuwa katika kutulia na kutumaini, lakini hamkubaali. Bali ninyi mlisema, La! Maana tutakimbia juu ya farasi; basi ni kweli mtakimbia; tena, sisi tutakimbia juu ya wanyama waendao upesi; basi wale watakaowafuatia watakuwa wepesi.*"

Hivyo hata leo, Mungu anatutaka tuweke tumaini letu kwake.

- Yakobo 4:8, "*Mkaribieni Mungu naye atawakaribia ninyi. Itakaseni mikono yenu enyi wenye dhambi, na kuisafisha mioyo yenu enyi wenye nia mbili.*"
- 1 Pet. 5:6-7, "*Basi nyenyekeeni chini ya mkono wa Mungu ulio hodari, ili awakweze kwa wakati wake; huku mkimtwika yeye fadhaa zenu zote, kwa maana yeye hujishughulisha sana kwa mambo yenu.*"

Ukweli wa jambo ni…

SIYO "*Mungu saidia wale wanaojisaidia wenyewe*"; bali, Mit. 3:5-6, "*Mtummaini BWANA kwa moyo wako wote, wala usizitegemee akili zako mwenyewe; katika njia zako zote mkiri yeye, naye atayanyoosha mapito yako.*"

Tunapomwacha Mungu nje ya maandiko katika kusuluhisha matatizo yetu, kitu kimoja hutokea: Mungu hutuacha ili tutatue matatizo hayo wenyewe, na bila msaada wake!

Kitu kingine kinawezekana: katika tendo la kupenda nidhamu, Mungu anaweza kushtukiza juhudi zetu katika kusuluhisha matatizo yetu kutegemea neno lake (ndivyo alivyowaadhibu Waisraeli!

Hitimisho

Hivyo tujifunze kwa mwenye ujuzi wa kushughulikia matatizo – Daudi.

Wakati wa shida, mtazame Bwana kwa ajili ya kukutia nguvu! Mtumaini Bwana na usimame imara katika kumtukuza na kumwomba. Usimwache, au kusanyiko la watakatifu ambayo hufanya tunamsogelea.

Kile ambacho Daudi amesema kumhudu iwe kweli kwetu pia: Zaburi 63:8, "*Nafsi yangu inakuandama sana; mkono wako wa kuume unanitegemeza.*"

Kumbuka kwamba wale wanao mtumainia Mungu watapata nguvu, kuokolewa, na furaha ya kweli!

Je unamwamini Bwana? au unaamini katika uwezo wako? Mwache Bwana awe mkombozi wako! Hasa inapotokea tatizo la hatia ya dhambi.

Mtu anaondokana vipi na hatia na kufanyika Mkristo? Zifuatazo ni hatua muhimu zinazofanya hilo liwezekane:

- **Imani.** Waeb. 11:6, "*Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza; kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko, na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao.*" Nilipokuwa shuleni (nikiwa na miaka 17), kijana mmoja jirani yangu, umri sawa na wa kwangu alikuwa haamini kuwa Mungu yupo. Kwa vile nilikuwa nimeshabatizwa, nilichukua nafasi ya kuongea naye ana kwa ana kuhusu maandiko. Akaniambia kwamba anaweza kuona kwamba kuishi maisha ya Ukristo ili kuwa ni nzuri. Lakini ili kuwa upande ambao ni salama, labda anaweza kwenda kanisani, na kama akifa na kusimama mbele za Mungu (kama kuna Mungu) siku ya hukumu (kama kuna hukumu), labda kama Mungu akiona kuwa amekwenda kanisani na kuishi maisha mazuri na kwamba Mungu atamruhusu kuingia mbinguni (kama kuna mbingu), na siyo motoni (kama kuna moto). Nikamwambia, "mambo haya hayafanyi kazi kwa njia hiyo. Lazima umwamini yeye kwa moyo wako wote, la sivyo huwezi kumpendeza."
- **Toba.** Matend. 2:38, "*Petro akawambia, tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu katika jina la Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*" Matend. 11:18, "*...Mungu amewapa pia mataifa toba liletalo uzima."* Kama ulikuwa una lala, ukasikia kelele katika chumba kingine, na unafikiria mwenyewe, "kuna mwizi ndani humu!" unachukuwa simu na taratibu unawapigia polisi, ukiwambia kwamba kuna mwizi ndani kwako, na unawapa anwani ya nyumba yako. Kidogo, unawasikia wanafika na kumkamata mwizi. Anapiga kelele, "samahani; samahani!" anaomba msamaha wa nini? Anaomba msamaha kwa sababu amekamatwa; na siyo kwamba ameiba. Katika toba ya kweli mwizi angeomba msamaha kwamba hataiba tena na anataka kubadilisha maisha yake ili kwamba asiibe tena. Ni badiliko la akili linalo leteleza badiliko la matendo. Hicho ndicho tunachotakiwa kukifanya kabla hatujawa Wakristo.

- **Kukiri.** Warumi 10:9-10, "*Kwa sababu ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. Kwa maana kwa moyo mtu huamini hatakupata haki, na kwa kinywa hukiri hatakupata wokovu.*" Tunakiri nini? Kwamba tunaamini kwamba Yesu Kristo ni mwana wa Mungu.

  Kumbuka kwamba katika somo hilo hapo juu imani (kuamini), toba na kukiri ni "**KATIKA**" haki, uzima, au wokovu. "Katika" humaanisha kuelekea kitu fulani; si kwamba mtu tayari ameshapata.

- **Ubatizo.** Ni katika ubatizo ndipo haki inapatikana, uzima, na wokovu vinapatikana. Yesu, mwenyewe, alibatizwa ili kuitimiza haki yote, "*Lakini Yohana alitakakumzuia, akisema, mimi nahitaji kubatizwa na wewe, nawe waja kwangu? Yesu akajibu akamwambia, kubali hivi sasa kwa kuwa ndivyo itupasavyo kuitimiza haki yote. Basi akamkubali. Naye Yesu alipokwisha kubatizwa alipanda kutoka majini, na tazama mbingu zikamfunukia, akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua akija juu yake; na tazama sauti kutoka mbinguni ikisema, Huyu ni Mwanangu, mpendwa mpendwa wangu ninayependezwa naye*." (Math. 3:14-17). Yesu alibatizwa kwa sababu Mungu alisema ni kitu sahihi ya kufanya. Unaona ni jinsi gani ilivyompendeza Mungu wakati Yesu alipobatizwa? Yesu pia alisema "*imekuwa kwetu **sisi** kuitimiza haki yote."* Tunabatizwa kwa sababu inatimiza haki yake yote, siyo kwa sababu ni haki yetu.

  Hakika, tusipobatizwa, bado tupo katika dhambi zetu. "*Petro akawambia, tubuni makabatizwe kila mmoja wenu kwa jina la Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*" (Matend. 2:38). Petro, ulisema ubatizo ni kwa ajili ya nini? "*Kwa ajili ya ondoleo la dhambi.*" Kwa nini mtu mwingine anaacha hatua hii muhimu inayoondoa dhambi zetu?

  Yesu aliamuru kwamba ili kuufikia wokovu ni lazima tubatizwe. "*Akawaambia, enendeni ulimwenguni mwote mkahubiri injili kwa kila kiumbe. Aaminiye **na** kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumiwa.*" (Marko 16:15-16).

  Anania alimwambia Sauli (kabla hajaitwa Paulo) kitu kama hiki, "*Sasa unakawilia nini? Simama, ukabatizwe uoshwe dhambi zako, ukiliitia jina la Bwana.*" (Matend. 22:16). Ubatizo ni agizo lililotolewa na Mungu.

Ubatizo unaitwa maziko. "*Hivyo mnazikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake: kama vile Kristo alivyofufuka katika wafu kwa utukufu wa Baba, hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima."* (Waru. 6:4). Utu wetu wa kale ni lazima ufe. *"Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima. Kwa maana kama mlivyounganika naye katika mfano wa mauti yake, kadhalika mtaungana kwa mfano wa kufufuka kwake; mkijua neno hili, ya kuwa utu wetu wa kale ulisulubishwa pamoja naye, ili mwili wa dhambi ubatilike, tusitumikie dhambi tena."* (Rum. 6:3-6). Ubatizo ni ramani ya Mungu kwa kutumia damu ya Kristo katika maisha yetu kwa njia ya ubatizo. Tunakuwa huru kutoka katika dhambi zetu za zamani pale tu tunapobatizwa.

Hii haimaanishi "kunyunyiza. Andiko hapo juu inasema ubatizo ni maziko. Hatuendi makaburini na kuchukua udongo kidogo na kuweka juu ya mwili wa marehemu.

Kama hujafanyika mshiriki wa kanisa la Kristo, kwa nini usizingatie leo"